
*KISWAHILI - "The Two Roads"*

# NJIA MBILI



## KUCHAGUA NJIA

Tuanzapo safari kwenda mahali ambapo hatujafika kabisa, tunauliza tusafiri njia ipi. Tunasafiri macho yetu yakiwa makini kabisa na tuonapo kwamba tuko kwenye njia ya uongo, tunageuuka na kutafuta njia sahihi, yaani ya kweli.

Kila siku wewe na mimi tunasafiri hapa duniani tukielekea kwenye uzima wa milele – usiomalizika, wala kubadilika mara tufikapo katika safari yetu. Je, wafahamu unaelekea wapi?.

## KITABU CHETU CHA KUTUONGOZA

Mungu, katika upendo na huruma zake, ametupatia kitabu cha kutuongoza, Biblia, ambacho chaonyesha wazi kabisa njia ya kwenda mbinguni. Maneno ya ujumbe huu yamenukuliwa katika Biblia (Zaburi 119:105) "Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu."

## NJIA PANA

Kuna umati wa watu katika njia hii. Mathayo 7:13 "Ingieni kwa kupitia mlango

ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo."

Wengi wanakuwa wamefumba macho. Hawajui, wala hawajali kwamba wanasafiri katika njia ielekeayo katika upotovu na uharibifu. Mithali 14:12 "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia ya mauti." 2 Wakorintho 4:4 "Ndani yao (akili yao) Mungu wa dunia hii (shetani) amepofusha fikira zao wasioamini."

## MIZIGO

Watu katika njia hii wamelemewa na mizigo ya dhambi. Warumi 3:23 "Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Hatuwezi kuficha hata dhambi moja mbele za Mungu. 1 Samweli 16:7 "Bwana (Mungu) haangali i kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Mungu huutazama moyo." Mizigo imefungiwa kwenye migongo yao. Huwezi kuwa huru kutokana na dhambi yeyote ile (hata ingalikuwa dhambi moja tu) kwa jitihada yako mwenyewe. Mzigo unaendelea kuwa mzito kila wakati unapoendelea, Warumi 6:23 "Mshahara wa dhambi ni mauti."

## NGURUMO

**Mwangaza** (unapotokea kabla ya radi) ni mfano wa **hukumu** ya Mungu. Waebrania 9:27 "Kufa mara moja, na baada ya kufa **hukumu** – (ya Mungu)." Ufunuo wa Yohana 20:11,12,15 "Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake... Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu... na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."

## MOTO

Kwa vile Mungu ni Mtakatifu na nwenye haki, lazima kuwe na adhabu ya dhambi. Nene la Mungu linatuambia kuwa kuna jehanamu mahali pa mateso milele, kwa wale wasiomtii Mungu. Biblia inatuambia, Wafilipi 3:19 "Mwisho wao ni uharibifu, Mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya dunia." Bali Mungu pia ni Mungu wa upendo, 2 Petro 3:9 "Hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba." Mungu, katika wingi wa huruma zake na upendo, ametengeneza njia ya kuepuka kwao wanaomhitaji kikamilifu (kweli kweli). **Je, unahitaji kutafuta njia hii ya uzima?**

## NJIA YA UZIMA – MWOKOZI

Kwa vile hatuwezi kujiweka huru wenyewe kutoka dhambi, au adhabu ya haki tunayostahili kwa ajili ya dhambi zetu, Mungu ametuletea Mwokozi, Yohana 3:16 "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanae pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Mungu, Baba yetu wa mbinguni, alimtuma Mwanae pekee, Bwana Yesu Kristo, toka mbinguni hadi hapa duniani. Aliishi kama binadamu, lakini hakutenda dhambi kamwe. Alitembea kila mahali akitenda mema; kuponya wagonjwa, kuponya wakoma, kutoa pepo, kusamehe wale wanaojuta kwa ajili

ya dhambi zao na kufundisha watu kuhusu Mungu.

Lakini jambo muhimu alilolijia kama mwanadamu ni kufa ili atoe uhai wake kwetu sote; kutoa damu yake takatifu - yenye thamani kubwa ili kulipa gharama ya dhambi zetu. Aliwaacha na kuruhusu waovu wamchukue, wakampiga mijeledi hadi mgongo wake ukatapakaa damu, wakamvika taji ya miiba kichwani, mwisho wakampigilia misumari msalabani (kumsulubisha), alitundikwa msalabani akiwa na maumivu makali mno, 1 Petro 2:24 "Yesu alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya msalaba." Alikufa kwa ajili yako na mimi.

## KUFUFUKA KWA YESU KRISTO

Baada ya kukaa siku tatu kaburini, Yesu Kristo alifufuka kutoka wafu. Alitembea na kuongea na wanafunzi wake, na baada ya siku arobaini alipaa mbingun na kuketi mkono wa kiume wa Mungu, Warumi 8:34 "Mwokozi anayeishi, na Kristo ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, maye yuko mkono wa kuume wa Mungu, tena ndiye atuombeaye." Mathayo 28:18 "Nimepewa (Yesu) mamlaka yote mbinguni na duniani." Pia Waebrania 7:25 "Aweza (Yesu) kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombee."

## MBINGUNI

Mbinguni ni mahali Mungu anapoishi katika utukufu wake. Yesu Kristo alisema Yohana 14:2,3 "Naenda kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo."

Ni mahali pa ajabu mno, ambapo Ufunuo wa Yohana 21:4,22:5 "Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwepo tena; Kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." "Wala hapatakuwa na usiku tena. ...kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru." Ni mahali patakatifu. Ufunuo wa Yohana 21:27 "Na ndani yake hakitaingia kamwe choohote kilicho kinyonge, wala yeye aganyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo."

Kuna njia moja tu ya kwenda mbinguni. Yohana 14:6 "Mimi (Yesu) ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba (Mungu), ila kwa njia ya mimi." Mtendao ya Mitume 4:12 "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."

## JINSI YA KUANZA NJIA YA KWENDA MBINGUNI

**1.** Marko 1:15 "Tubuni, na kuiamini Injili."
**2. Njoo kwa Yesu Kristo,** katika maombi, kama ulivyo na mizigo yako ya dhambi na mwombe Yesu akusamehe dhambi zako. Yesu asema, Matayo 11:28 "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha."
**3. Amini Kristo pekee kwa ukombozi toka katika dhambi.** Waraka wa kwanza wa Yohana 1 Yohana 1:7 "Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi zote."
**4. Yesu atakupa maisha mapya... na uzima wa milele.** Kristo alisema Yohana 5:24 "Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka, yuna **uzima**

**wa milele"** wala haingiii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. 2 Wakorintho 5:17 "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya."

**5.** Utakuwa na amani moyoni. Warumi 5:1 "Tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo." Waraka wa kwanza wa Yohana 1 Yohana 5:11-13 "Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele na uzima huu ume katika Mwanawe. Yeye aliye na Mwana (Yesu), anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima. Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mlioliamini jina la Mwana wa Mungu.

**JINSI YA KUISHI MAISHA MAPYA**

**1. Soma Biblia kila siku.** Pamoja na kuwa mwanga katika njia zetu, ni chakula kwa roho zetu. 1 Petro 2:2 "Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu." Mwombe Mungu akuongoze na kukufundisha kwa uwezo wa roho wake Mtakatifu jinsi unavyoendelea kusoma (kujifunza).

**2. Karibia Mungu kwa sala (maombi) kila siku,** omba katika jina la Yesu. Wafilipi 4:6.7 "Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."

**3. Eleza (shuhudia) wengine habari za Yesu kwa watu wa kwenu,** kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana (Mungu) na jinsi alivyokurehemu.

**4. Katika majaribu – Mwite Yesu.** Waebrania 2:18 "Na kwa kuwa mwenyewe (Yesu) aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa."

**5. Kama utatenda dhambi tena, tubu haraka (mara moja) kwa Mungu.** 1 Yohana 1:9 "Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki haja atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

**6. Jaribu kuambatana na waumini wengine (walokole – waliozaliwa mara ya pili) ndani ya Bwana Yesu Kristo.** Yohana 15:12 "Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi."

---

Kindly write to us if you are able to assist us with further translations of our free Gospel literature, informing us of the language into which you could translate this Gospel literature. Your assistance would be appreciated.

**Our Heart of Man Book can now be downloaded in 480 different languages onto cell phones, tablets, etc from our website www.angp-hb.co.za.**

If you have found salvation in Christ, or have been otherwise blessed through our Gospel literature, please let us know. We would like to thank God with you, and remember you further in our prayers.

For **free** Gospel literature, books and tracts in over 540 languages, write to:

**E-MAIL: info@angp.co.za**

**ALL NATIONS GOSPEL PUBLISHERS**

**P.O. Box 2191, PRETORIA, 0001, R.S.A.**

(A Gospel Literature Mission financed by donations)

(Reg. No. 1961/001798/08)